# NGUVU YA KUSHINDA MAZINGIRA (ADUI) IMO KATIKA KINYWA CHANGU PALE NINAPOTAMKA NENO LA USHINDI MBELE ZA ADUI.

**Maandiko: ZAB. 108:13, 2Timoth 4: 18 NA WAFILIPI 4: 13**

## 1. UTANGULIZI

Yesu wakati anatoa taarifa ya kumaliza kazi aliyotumwa na Baba yake aifanye hapa duniani katika **Yohana 17: 1 – 19** hakutuficha kwamba alipotuokoa sisi sote ametuacha katika Ulimwengu huu na mazingira yake; na kama yeye alivyokaa katika Ulimwengu huu na mazingira haya akashinda; nasi lazima katika Ulimwengu huu na mazingira haya tuishi maisha ya ushindi daima kama yeye alivyoishi na kushinda.

- Tangu siku tulipookoka tu, tulitangaza vita na shetani mpaka tutakapoondoka katika Ulimwengu huu na mazingira haya; na wakati wote tuwapo vitani na ibilisi, Mungu anatutaka tukiri Neno na uwezo wake (ukuu wake) mbele za adui!!! **Hii ni siri ya ajabu na ya kushangaza sana ambayo imefichika mno!!! "Pale tunapokiri Neno la Mungu na uweza (ukuu) wa Bwana Yesu mbele ya adui (shetani), Mungu husimama saa hiyo hiyo na kuingia vitani kwa niaba yako!!! Kwa maana nyingine nzuri zaidi tayari unakuwa umemuuzia kesi yako Bwana Yesu ya kupigana vita hiyo kwa niaba yako hadi atakapoimaliza. Na kwa kweli vita yetu na ibilisi siyo yetu hasa 2Nyak. 20:15 ni vita vya Bwana Yesu na shetani**.
- **Ndiyo sababu kila mteule analazimika kulinda sana moyo wake kuliko vitu vingine vyote anavyolinda maana ushindi wa kila mteule dhidi ya adui shetani unaanzia ndani ya moyo wake!!! Mith. 4: 23. (na kitu kikubwa kinachofanya moyo wa mteule uwe salama ni**

**kuujaza Neno la Mungu wakati wote. Zab. 119: 11, Luk. 2: 16 – 19.**

2. Kinywa (mdomo) wa mtu hunena yale yaliyojaa ndani ya moyo wake. **Mark. 7: 20 – 23** (nifafanue), kinywa ni kama **tape** ya bomba la maji ambalo limeunganishwa kutoka katika chanzo maalumu cha maji hayo!!!

- **Kinywa** - tape maalumu ya bomba la maji

- **Moyo** – chanzo maalumu cha maji (labda niite chanzo hicho ni mto au ziwa au kisima)
- Moyo unapokuwa umejaa Neno la Mungu, kinywa kitatamka Neno hilo lililojaa moyoni saa unapokuwa katika uwanja wa vita na shetani.

- Ngoja nifafanue jambo hili zaidi kama mtume Yakobo alivyofafanua – ***Yak. 3: 1 – 12.***
  ***Ninapokuwa naendesha gari langu; (dereva) lazima nikamate usukani.***

- **Usukani** uko ndani ya kila gari, lakini kama **dereva** hayupo, **usukani** hauna maana yoyote, na hata kama **dereva** akawepo na kuendesha gari hilo kwa kutumia **usukani** huo, na gari likaacha njia na kuelekea kusikopasa, wa kulaumiwa siyo **usukani** bali wa kulaumiwa ni **dereva!!**

  "**Sasa katika maisha ya wokovu= moyo (mawazo & fikira zetu) ndiyo dereva, na ulimi unabaki kuwa kama usukani** tu, wa kulaumiwa daima ni moyo (mawazo & fikira). **Math. 5:27-28, Luk. 6:45** na ndiyo Mfalme Sulemani akasema hivi. **Mith. 18:20-21**. **Kama kwenye moyo wa mteule kutajaa Neno la Kristo. Zab. 119:11, Yosh. 1:8, Kumb. 17:14-20, Zab. 1:1-2 yeye kushinda vita wakati wote ni lazima maana wakati wote wa vita vyake na ibilisi yeye atatamka Neno la Mungu, na Yohana alipotaja**

**siri tatu za ushindi wetu katika ufunuo 12: 11 alisema "Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana – Kondoo (Yesu) na kwa Neno la ushuhuda wao ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"**

- Ukikuta mtu anasema ameokoka lakini anapenda kusema uongo, kusengenya au kutukanatukana watu uelewe wazi kwamba ndani ya moyo wake haya ndiyo yaliyojaa kama Yesu Kristo alivyofundisha katika **Luk. 6:43-45 (Hakuna kabisa mti mzuri uzaao matunda mabaya wala mti mbaya uzaao matunda mazuri!!** Hoja zenye nguvu saa zote tunapokuwa vitani na ibilisi, ni hoja zinazohusisha Neno la Mungu pamoja na ahadi zake. **Isay. 41:21**

3. Somo letu maalumu sana leo ni nguvu ya kushinda mazingira (adui) imo katika kinywa changu pale ninapotamka Neno la Kristo la ushindi mbele za adui ninaokabiliana nao; na baada ya kutoa maelezo ya msingi sana katika utangulizi ili nilete uelewa wa kina sana kwa watoto wa Mungu, sasa tuangalie mifano michache ya wateule waliotutangulia na wakashinda kabisa tukimwacha Yesu Kristo ambaye ushindi wake pale msalabani na baadaye kufufuka siku ya tatu kulimwacha shetani na wapambe wake midomo wazi!!
   a. Saa ya vita kati ya Musa na Farao pamoja na majeshi yake **Kut. 14:10-14. Musa aliposema neno la Bwana** lililotoka ndani ya moyo wake kabisa **(mst 13-14).** Tayari alikuwa amemuuzia Mungu Baba kesi yote na ndipo Bwana wa vita alipoingilia kati na kuimaliza vita hiyo yeye mwenyewe. **Kut. 14:15-31.**
   b. Ona Mfalme Daudi alivyochora picha nzuri sana ya ukuu wa Bwana Yesu ndani ya moyo wake kwanza. **Zab. 27:1-6,** hata Goliath alipokabiliana na Daudi akiwa na picha hii moyoni mwake, Mfalme Daudi alisema " **1Saml. 17:45-47. (Tusome wote)**

Hii ilikuwa ni kauli iliyomfanya Mungu Baba asimame haraka na kumshughulikia Goliath kwa niaba ya Daudi na kwa niaba ya Taifa zima la Israel.

c. Mfalme Yehoshafati yeye alimuuzia Mungu Baba kesi yake na majeshi ya wana wa Moabu na Amoni na Wameuni yaliojipanga kupambana naye kwa stahili ya aina yake. **2Nyak. 20:1-12** (Yehoshafati alifanya mambo makuu matano (5)

i. Alijinyenyekesha yeye na watu wake ili wamtafute Bwana. **Mst 3-4. Aliweka kando uzoefu wake wa kupigana vita na kutotegemea mali na utajiri mwingi sana aliokuwa nao. 2Nyakt. 17: 5; 18:1**

ii. Yehoshafati alimsifu Mungu na kutaja ukuu wake kwamba ndiye anayetawala Mbingu na nchi na Falme zote na Mataifa yote. **Mst 5-6- Mungu anapenda sana kusifiwa na kutukuzwa daima (Isay. 42: 8)**

iii. Yehoshafati alimkumbusha Mungu matendo yake makuu ambayo aliwatendea Wana wa Israel pamoja na kuwafukuza Wafilisti (wenyeji) wa nchi wanayoikaa na kuwapa wao!! **Mst. 7-8- Isay. 43: 26- Waone Wawakili mahakamani; siyo kwamba Jaji hajui vifungu vya sheria; lakini kazi ya Mawakili ni kumkumbusha vifungu vya sheria.**

iv. Yehoshafati akamkumbusha Mungu maneno aliyomwambia Mfalme Suleimani siku ya kuzinduliwa kwa hekalu takatifu alilolijenga Mfalme Suleimani**. 2Nyak. 20:8-9, (2nyak 7:12-18)**

v. Yehoshafati akamwonyesha Mungu tatizo walilokuwa wanakabiliana nalo na kukiri mbele yake kwamba wao

hawana uwezo nalo na wala hawajui la kufanya; isipokuwa sasa wanamwangalia yeye anayejua la kufanya!! **2Nyak. 20:10-13** (Hapa Mungu Baba akauziwa kesi yote na Yehoshafati na yeye bila kuchelewa akasimama na kuingia vitani kwa niaba ya Yehoshafati na Taifa zima la Yuda **2Nyak. 20:22-30 Haleluya.**

4. Tumalize somo letu hili muhimu sana na maalumu mno juu ya ushindi wa mazingira (adui) tunaekabiliana naye kila siku kwamba upo katika vinywa vyetu pale tunapokiri neno la Mungu na ukuu wake mbele za adui kwa kuwataka kila mmoja wenu kila anapoamka asubuhi na kufanya maombi yake; **ahakikishe ana riziki ya Neno la Mungu ya siku hiyo (Math. 6:11) yaani mstari wa moyo atakaotembea nao na kushinda nao**.

   ***Mfano***

   i. Labda umeamua kutembea na **1Petr. 1:5** (mimi ninalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya Imani) hadi nitakapopata wokovu mkamilifu siku Bwana Yesu atakaporudi kunitwaa kutoka katika dunia hii mbovu!! Kutembea na kuimba mstari huu kutoka ndani ya moyo wako kutapelekea Mungu Baba aagize ulinzi usio wa kawaida ukuzunguke saa zote na pande zote.
   ii. **Au tuseme riziki yako ya moyo ni Isaya 54:10** mstari huu unasema “maana milima itaondoka na vilima vitaondolewa, bali wema wangu hautaondoka kwako,wala agano langu la amani halitaondolewa, asema Bwana akurehemuye; Kusema tu mstari huu mara kwa mara ndiko kunakojenga picha nzuri mno ya Mungu Baba kuhusu wema wake ndani ya moyo wako jambo ambalo linamfanya Mungu naye ahakikishe wema wake kwako

haupungui maadamu analiangalia Neno lake wakati wote ili apate kulitimiza. **Yer. 1:12.**

iii. **Au tuseme kwamba riziki yako ya moyo siku ya leo ni Isaya 54:17.** Kila silaha itakayofanyika juu yangu leo haitafanikiwa; na kila ulimu utakaoinuka juu yangu katika hukumu (kunilaani au kuzuia Baraka zangu) Bwana Yesu mwenyewe atahukumu kwa sababu umekosea mtu wa kumlaani maana mimi ni Mbarikiwa, mimi ni mtumishi wa Bwana Yesu niliye na haki zote za kubarikiwa!! Tayari kwa mstari huu tu, kamwe hakuna atakayekuondolea Baraka zako na laana zote hakuna hata moja itakayokupata.

**Mwisho:**

Maadamu tuliookoka, tumembeba Mungu wa dunia nzima mioyoni mwetu (**Yosh. 3:13, 1Kor.3:16, Yoh. 14:23** nataka niwaambie leo Neno la Mungu muhimu sana tunapomaliza mwaka 2022 kwamba **"Isay**. **41:8-16** kuanzia sasa, asiwepo mwana Sayuni anayemwogopa tena adui shetani wala mazingira anayokabiliana nayo kwa sasa katika maisha haya; Bwana Yesu asimame na kumshika mkono na kumsaidia kuvuka salama 2022. Na woote walioona hasira juu yako watataharika na mwaka kesho utawatafuta wala hutawaona tena milele asema Bwana wa majeshi na kuanzia sasa na kuendelea, Bwana Yesu akufanye kuwa chombo chake maalumu tena chenye meno tayari kwa **kufikicha** kila aina ya milima (matatizo yote yanayopangwa na adui) na kuyatupa baharini kwa Jina la Yesu Kristo. **Mark. 11:23-24 na Isay. 41:8016. Amina**

***Na***
***Ask. Dr. L. M. Mwizarubi***
***04/12/2022***